JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UCHUKUZI

MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI

# TAARIFA KWA UMMA

## LATRA INAENDELEA KUTEKELEZA MAJUKUMU YA UDHIBITI KWA MUJIBU WA SHERIA

***Morogoro, Tarehe 16 Juni, 2025.***

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) inautaarifu Umma kwamba, tarehe 05 Juni, 2025, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilipitisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria mbalimbali, ikiwemo Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura ya 413 na Sheria ya Utoaji wa Leseni Sura ya 317.

Marekebisho hayo yameondoa majukumu ya Ukaguzi wa Utimamu wa Magari (roadworthness) na Uratibu wa shughuli za Usalama wa Usafiri Ardhini katika Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini. Ukaguzi wa Magari ulioondolewa ulikuwa unalenga kuwa na mfumo wa kisasa wa ukaguzi wa lazima wa magari yanayotoa huduma kibiashara kabla ya magari hayo kupewa leseni za LATRA.

Marekebisho haya ni matokeo ya mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai ambayo, pamoja na mambo mengine, ilibainisha kuwepo kwa muingiliano wa majukumu kati ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura ya 413 na Sheria ya Usalama Barabarani Sura ya 168 inayotekelezwa na Jeshi la Polisi. Kabla ya marekebisho haya, ukaguzi wa magari umekuwa ukifanywa na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani ambalo linaendelea na majukumu hayo baada mabadiliko haya ya Sheria.

Pamoja na marekebisho, LATRA inaendelea kutekeleza majukumu mengine yote yakiwemo kutoa Leseni, kuthibitisha madereva, kusajili wahudumu na kusimamia utekelezaji wa masharti ya leseni.

Mamlaka inawakumbusha wadau kuwa, kusambaza taarifa zisizo na ukweli zinazolenga kupotosha Umma ni kosa kwa mujibu wa Sheria.

Digitally Signed By Salum PAZZY
Mon Jun 16 18:06:19 EAT 2025

Salum PAZZY

**Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano**

LATRA Makao Makuu, S. L. P. 1742, 41104 Tambukareli, Dodoma
Simu + 255 262 323 930, Barua pepe: dg@latra.go.tz , info@latra.go.tz , Tovuti: www.latra.go.tz